TANGAZO LA SERIKALI NA.174 la tarehe 17/3/2023

SHERIA YA MIPANGO MIJI,
(SURA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1)*

AMRI YA KUPANGA ENEO LA BUGOMBA YA MWAKA 2023

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kupanga Eneo la Bugomba ya Mwaka 2023.

Utangazaji wa eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango Miji.

Mpango katika eneo la kwenye Jedwali

3. Mipango ya jumla na kina katika eneo lililoainishwa katika Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu.

## JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

"Mpaka unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba SHV 475 yenye majira – nukta 395294MS, 9558754KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki katika uelekeo wa KS56°33'32"MS kwa umbali wa kilomita 3.52 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba SHV 474 yenye majira – nukta 398171MS, 9556797KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki katika uelekeo wa KS84°34'25"MS kwa umbali wa kilomita 1.49 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba SHV 485 yenye majira – nukta 399651, 9556910; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini katika uelekeo wa KS17°45'36"MS kwa umbali wa kilomita 1.72 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba SHV 472 yenye majira - nukta 400141MS, 9555289KZ; baada ya hapo mpaka

*Tangazo la Serikali Na. (Linaendelea)*

unaelekea Kusini - Magharibi katika uelekeo wa KS39°11'25"MG kwa umbali wa kilomita 5.7 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba SHV 473 yenye majira – nukta 396525MS, 9550823KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi katika uelekeo wa KS61°24'54"MG kwa umbali wa kilomita 1.43 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba SHV 532 yenye majira - nukta 395328MS,9551503KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi katika uelekeo wa KS88°46'53"MG kwa umbali wa kilomita 1.08 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba SHV 483 yenye majira - nukta 394294MS, 9551534KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi katika uelekeo wa KS87°21'01"MG kwa umbali wa kilomita 2.59 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba SHV 484 yenye majira - nukta kwenye majira nukta 391673MS, 9551667KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea kwenye alama ya mpaka namba SHV 482 yenye majira - nukta 387833MS, 9551910KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki katika uelekeo wa KS19°58'35"MS umbali wa kilomita 3.68 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba SHV 476 yenye majira - nukta 389094MS, 9555418KZ; baada ya hapo mpaka unafuata mto Mwasengela katika uelekeo wa KS76°29'18"MS kwa umbali wa kilomita 5.67 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba SHV 477 yenye majira - nukta 394587MS, 9556733KZ; hadi ulipoanzia''

Dodoma,
6 February, 2023

ANGELINE S. MABULA
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*